

# Athari za Mchakato wa Utwaaji Ardhi kwa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kwa Jamii Wilaya ya Kiteto, Mkoa wa Manyara

KINNAPA Development Programme  
Juni 2024

## Muhtasari

Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) ni mradi wa kusafirisha mafuta ghafi kutoka katika fukwe za Ziwa Albert nchini Uganda hadi Bandari ya Tanga nchini Tanzania. Mradi huu kwa hapa Tanzania utapita katika mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Dodoma, Manyara na Tanga. Mradi huu mkubwa unatarajiwa kupita katika Wilaya ya Kiteto iliyopo katika Mkoa wa Manyara nchini Tanzania. Ujenzi na uendeshaji wa bomba hili utakuwa na athari kubwa kwa jamii katika Wilaya ya Kiteto, hasa kutokana na taratibu zinazohitajika za upatikanaji wa ardhi litakapopita bomba na athari za kijamii na kimazingira zinazoweza kutokana na utekelezaji wa mradi huu. Shirika la KINNAPA lilifanya utafiti mdogo ambao ulilenga kutathmini athari za michakato ya utwaaji ardhi kwa mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kwa jamii wilayani Kiteto, mkoani Manyara. Malengo mahususi ya utafiti huu yalikuwa 1; Kutathmini mchakato wa utwaaji ardhi katika wilaya ya Kiteto (kwa kulenga vijiji 3), 2; Kutathmini mitazamo ya jamii kuhusu fidia inayohusiana na mchakato wa utwaaji wa ardhi wa EACOP, 3; Kutathmini uelewa wa watu walioathirika na mradi wa EACOP na 4; Kutathmini ushiriki wa wafugaji, wawindaji na wakulima wa mazao katika mchakato wa EACOP wa kutwaa ardhi. Tathmini ilifanywa kupitia mchanganyiko wa tafiti za maeneo, mahojiano, na ushirikishwaji wa jamii ya watu walioathirika na mradi katika vijiji vya utafiti vya Loolera, Kimana na Ndorkon.


Utafiti unaonyesha matokeo muhimu yafuatayo. Kwanza, mchakato wa utwaaji ardhi ulifuata mfumo wa kisheria na ulizingatia matakwa ya sheria za ardhi za Tanzania zilizowekwa kwa ajili ya utwaaji wa ardhi kwa lazima kwa matumizi ya umma. Ingawa wengi wa waliojibu walichukulia fidia kuwa

ya haki, pia kulikuwa na wasiwasi uliotolewa kuhusu haki, utoshelevu na fursa za mazungumzo ya kulipwa fidia. Mchakato wa fidia kwa ardhi ya jumuiya pia uliibua masuala, ukisisitiza haja ya uwazi katika upatikanaji wa ardhi kwa siku zijazo.

Pili, utafiti unaonyesha kiwango tofauti cha uelewa na maarifa kuhusu mradi wa EACOP kwa miongoni mwa watu walioathirika na mradi huo. Kwa ujumla, kuna upungufu mkubwa wa uelewa kuhusu athari za mradi na mikakati ya kuzuia athari hizo. Hii inaweza kuwa ni kutokana na idadi ndogo ya ushirikishaji wa jamii zilizoathirika na EACOP, na ukweli kwamba mazungumzo yalifanyika tu na viongozi wa vijiji na watu walioathirika lakini si na jamii yote ya vijiji ambavyo mradi EACOP na miundombinu yake itajengwa. Jamii pamoja na watu walioathirika na mradi wameachwa na maswali mengi na wasiwasi. Kimsingi wasiwasi umeangazia hatari inayoweza kutokea ya upotezaji wa ardhi ya kilimo cha mazao na maeneo ya malisho. Ni muhimu kwa michakato ya utwaaji ardhi kwa siku zijazo kuhakikisha uwazi, kufanya ushirikishaji mkubwa wa jamii zilizoathirika, na kuboresha mifumo ya mawasiliano na uhamasishaji na kushughulikia maswala ya jamii zilizoathirika.

Pamoja na hayo utafiti uligundua kuwa ushiriki wa makundi mbalimbali katika jamii zilizoathirika, kama vile wafugaji, wawindaji-waokota matunda na wakulima, katika ushirikishwaji umekuza mshikamano wa kijamii na umoja miongoni mwao. Kwa hivyo, ni muhimu kuhusisha na kuzingatia mitazamo ya makundi yote ya jamii yaliyoathirika ili kukuza usawa, ushirikishwaji, na uwiano wa kijamii katika michakato ya utwaaji wa ardhi.

Utafiti unahitimishwa kwa mapendekezo kadhaa kwa wadau mbalimbali, ikiwemo kuimarisha uwazi na mawasiliano ya mradi (kwa EACOP), kuwezesha ushirikishwaji wa jamii katika michakato ya utwaaji ardhi (kwa viongozi wa vijiji), kuimarisha mfumo wa kisheria wa utwaaji ardhi (kwa watendaji wa serikali), na kutetea maslahi ya jamii (kwa makundi kama vile wafugaji, wawindaji-waokota matunda, na wakulima). Utafiti unasisitiza umuhimu wa kuzingatia mitazamo yote ili kukuza usawa na uwiano wa kijamii katika michakato ya utwaaji ardhi.



mawasiliano  
[info@kinnapa.or.tz](mailto:info@kinnapa.or.tz)



**Belgium**  
partner in development

Kwa msaada wa **IPIS**

Chapisho hili ni sehemu ya mfululizo wa "Sauti za Watanzania" wa IPIS na toleo lake kuhusu "Athari za mikakati ya utwaaji ardhi katika sekta ya uziduaji kaskazini mwa Tanzania"

Ripoti kamili ya kifani hii inapatikana kwa Kiingereza kupitia: <https://ipisresearch.be/home/capacity-enhancement/voices-from-the-south/voices-from-tanzania/>